

MARA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKARI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MJI WA TARIME

Simu: +25528-2690218  
+255282690043  
Nukushi: +25528-2690218  
Barua pepe: td.tarime@mara.go  
.tz



Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji  
S.L.P 45,

Unapojibu tafadhari taja

08/11/2017.

TANGAZO LA UKODISHAJI WA JENGO LA MAMLAKA YA  
MAJI, HALMASHAURI YA MJI TARIME.


Kwa, WANANCHI WOTE.

1. Halmashauri ya Mji Tarime S.L.P 45 Tarime imeamua kubadili matumizi ya jengo lake la mamlaka ya maji na kulipangisha. Hivyo halmashauri ya mji Tarime inakaribisha maombi toka kwa makampuni, mashirika, vikundi na watu binafsi wenye nia ya kukodi jengo hilo.
2. Jengo liko katika barabara ya Nyerere mkabala na BSG pharmacy karibu na Benk ya NBC.

S/N	Maelezo	Idadi ya vyumba	Aina shughuli/biashara.
1.	Upangishaji wa jengo la mamlaka ya maji, Tarime mjini.	- Hall kubwa - vyumba vinne(4) vya ndani. - Sebule mmoja(1) kubwa -stoo. -Eneo la wazi kwa nyuma.	Unaruhusiwa kufanya shughuli zozote za kiuchumi au kijamii zinazokubalika kisheria.

MARA

3. Maombi yote yawe na nakala halisi (original) moja na nakala mbili zinazofanana, zilizojazwa kwa usahihi na zilizowekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi juu na kuandikwa **Maombi ya ukodishaji wa Jengo la mamlaka ya maji Halmashauri ya mji Tarime**. Ni lazima kupelekwa kwa **Mkurugenzi wa Mji Tarime S.L.P 45 Tarime, Ofisi ya Kitengo cha manunuzi**.
4. Vitabu vya maombi kwa Lugha ya **Kiswahili** vitanunuliwa na waombaji wanaohitaji kwa kuandika barua ya maombi kwa anwani iliyooneshwa kwenye aya ya 3 hapo juu kwa gharama ambayo haitarudishwa ya **Shilingi za kitanzania 50,000/ ambazo zitalipwa kwenye Bank ya NMB** baada ya kupata ankra na Namba ya Akaunti kutoka Idara ya Fedha ya Halmashauri ya Mji Tarime S.L.P 45 Tarime.
5. Siku ya mwisho ya kuwasilisha maombi ni Siku ya **Jumane Tarehe 21/11/2017** kabla ya Saa **7.00 Mchana**. Maombi yote yatafunguliwa hadharani mara tu baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha, mbele ya wawakilishi wa waombaji walioamua kuhudhuria katika kikao cha ufunguzi katika **Halmashauri ya Mji wa Tarime**.
6. Maombi yatakayochelewa, maombi ya kielektroniki na maombi ambayo hayajafunguliwa katika tukio la ufunguzi, kwa hali yo yote ile hazitakubaliwa kwa tathmini.

  
.....  
Pidas K. Masungwa  
**Kaimu Mkurugenzi**  
**Halmashauri ya Mji Tarime.**

**U.n.y. MKURUGENZI MTEMDAJI**  
**HALMASHAURI YA MJI**  
**TARIME**

